


UMESIMAMISHWA NA POLISI WAKATI UKIENDESHEA?

ZIJUE HAKI NA WAJIBU WAKO!



Kila mwananchi **anao** wajibu wa kusimamia na kutii kikanilifu sheria za nchi. Usalama barabarani ni jukumu la kila mmoja wetu, hivyo kutii sheria za barabarani iwe ni utamaduni kwa wananchi wote hususan madereva kwa lengo la kulinda maisha ya watu na mali zao. Tujijenge utamaduni wa kutii sheria bila kushurutishwa

Polisi wana kazi ngumu na muhimu sana ya kusimamia sheria. Lazima kushirikiana nao, isipokuwa kama wanatenda kinyume na sheria.

Maelezo hayo ni muhtasari wa mwongozo wa nini ofisa wa polisi aliyevaa sare anaweza kufanya kisheria na kukueleza ni wakati gani anakusimamisha uwapo barabarani. Unaweza ukapenda kukata maelezo haya na kuyaweka kwenye gari lako i *lakini kumbuka kwamba ni mwongozo tu.*

Mamlaka ya kusimamisha gari lako: Ofisa wa polisi ana haki ya kusimamisha gari lako i kama atakupa ishara ya kusimama, punguza mwendo kwa usalama na utoke barabarani i pia anaweza kukuuliza jina na anwani yako na ile ya mmiliki wa gari (Sheria ya Usalama Barabarani (RTA), s.78).

Leseni ya kuendesha gari: Ofisa wa polisi anaweza kuomba kuona leseni yako ya kuendesha gari i anaweza kukataa fotokopi i hata hivyo, unaweza kuamua kupeleka leseni yako ndani ya siku tatu kwenye kituo cha polisi kilichochaguliwa na ofisa. Ili kuepuka matatizo, wakati wote

tembea na leseni yako kwenye gari (RTA s.77).

Hati ya usajili: Ofisa wa polisi ana haki ya kukagua maelezo ya usajili kama yanavyoonyeshwa kwenye kibandiko cha usajili i gari lazima liendane na maelezo ya kwenye kibandiko, lakini vitu vidogo kama rangi iliyofifia au iliyobanduka haijalishi (RTA s.13).

Leseni ya barabarani, na bima ya gari: Ofisa wa polisi ana haki ya kukagua kama umebandika leseni halali ya barabarani na kibandiko cha bima kwenye kiwambo cha upepo cha gari lako (kioo che mbele).

Kunyang'anywa: Ofisa wa polisi HANA haki ya kuondoa vibandiko na kuchukua leseni isipokuwa kwa mujibu wa sheria.

Matumizi ya taa nyakati za usiku: Sheria ya usalama barabarani inakutaka kupunguza mwanga wa taa za gari lako unapopishana au kutaka kulipita gari la mbele yako ili kumwezesha dereva mwenzako kuyaona vizuri mazingira ya barabara anayotumia (RTA s.39).

Kuendesha baada ya kunywa pombe: Kama ofisa wa polisi anakuhihi umekunywa pombe na huwezi kulidhibiti gari ipasavyo, anaweza kukutaka upimwe (kipimo cha kupumua au kipimo cha damu) kuona kama kiasi cha pombe kwenye damu yako ni zaidi ya kiwango kilichoelezwa. Kama ukikataa utakuwa na hatia ya kosa (RTA s.44, s.45, s.46).

Kutumia simu ya mkononi wakati unaendesha: ingawa sheria haikatazi hili mahususi, ofisa wa polisi anaweza kuona

kuwa unatenda kosa la fkuendesha kwa uzembeo (RTA, s.42, s. 50).

Mwendo kasi: Unapaswa kuzingatia kikomo cha mwendo kasi, (ikiwa ni pamoja na km 50 kwa saa katika maeneo ya hatari, ambayo yanaweza yasiwe na alama) i ofisa wa polisi anaweza kupima mwendo kasi wako kwa namna mbalimbali - hata hivyo, unaweza kupinga ushahidi wake mahakamani (RTA s.51, s.73(2)).

Kustahili kuwepo barabarani: Ofisa wa polisi ana haki ya kukagua kama gari lako liko katika hali ya usalama kiufundi. Matairi, breki, taa, indiketa na usukani lazima viwe vinafanya kazi vizuri i unaweza kutakiwa kupeleka gari mahali litakapokaguliwa kikanilifu na mkaguzi wa magari wa polisi (RTA, s.39.1, s.81).

Unashauriwa kupeleka gari lako kukaguliwa na polisi kila mwaka. Pata stika ya usalama barabarani, cheti cha ubora wa gari, au barua kutoka polisi kama ushahidi kwamba gari lako limekaguliwa.

KAMA OFISA WA POLISI ANAKUTUHUMU KWAMBA UMEFANYA KOSA: Mara nyingi utapewa uchaguzi wa kukubali kosa na kulipa faini ya sh. 20,000 kwa ofisa wa polisi, au kwenda mahakaman ili kujibu mashtaka. Ofisa ataandika maelezo kwenye Fomu ya Polisi ya PF 101, na nyote wawili mtatia saini i kamwe usilipe faini bila ya kupata nakala ya Fomu iliyotiwa saini. Unaweza kwenda na ofisa kwenye kituo cha Polisi kutoa maelezo. Kama unakubali kosa, lakini huwezi kulipa

faini, ofisa wa polisi atakueleza jinsi ya kutuma malipo kwa kamanda wake wa eneo (RTA, s.95).

KAMA UNAFIKIRI OFISA WA POLISI AMETENDA KINYUME CHA SHERIA AU AMEKOSEA KWA NJIA YOYOTE UNaweza KUTOA MALALAMIKO: Muulize ofisa jina lake, cheo na namba, na anwani ya kituo cha polisi anakofanyia kazi (unayo haki ya kuuliza hilo.) Kisha peleka malalamiko ya maandishi kwa Mkuu wa Polisi wa eneo husika au kwa Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, S. L. P 1712, Dar es salaam i ambaye atachunguza na kujibu.

Tusaidie kuwafanya maafisa polisi wetu kuwa waaminifu – usitoe rushwa na usipokee rushwa.

Said A. Mwema

Inspekta Jenerali wa Polisi

10/6/2011

Jeshi la Polisi Tanzania na Wizara ya Ujenzi i wanashirikiana kwa ajili ya usalama zaidi wa barabara.

KATA NA WEKA KWENYE GARI LAKO

